

JEDWALI LA PILI
NAULI ZA MABASI YA MIJINI (DALADALA)

Na.	Umbali wa Njia	Nauli (SH.)
1	Usiozidi Kilomita 10	600
2	Kuanzia Kilomita 11 hadi 15	700
3	Kuanzia Kilomita 16 hadi 20	800
4	Kuanzia Kilomita 21 hadi 25	900
5	Kuanzia Kilomita 26 hadi 30	1,100
6	Kuanzia Kilomita 31 hadi 35	1,300
7	Kuanzia Kilomita 36 hadi 40	1,400

Nauli ya Mwanafunzi

Nauli ya mwanafunzi kwa mabasi ya mijini (daladala) kwa umbali wa njia zote itaendelea kuwa **shilingi 200 kwa kila safari**.

MAMBO YATAKAYOFUATILIWA NA LATRA

LATRA inawaelekeza watoa huduma wa usafiri wa mabasi ya masafa marefu na mijini (daladala) kuzingatia yafuatayo:

(a) Mabasi ya Masafa Marefu

- (i) Nauli zinazotozwa zisizidi ambazo zimetolewa kwenye Tangazo hili.
- (ii) Madereva na wahudumu (makondakta) kuvaa sare safi na nadhifu.
- (iii) Mtoa huduma kutotoza nauli zaidi ya umbali anaoenda abiria.
- (iv) Basi liwe safi wakati wote na kupuliza dawa ya kuua wadudu.
- (v) Kutumia mfumo unaoruhusu abiria kuchagua kiti na kukata tiketi mtandao.
- (vi) Kuweka alama kwenye mizigo (luggage tags) kuepuka upotevu.
- (vii) Kuwatumia madereva waliothibitishwa na LATRA.
- (viii) Kuhakikisha matumizi ya kitufe cha utambuzi wa dereva (*i-button*).
- (ix) Kutokuweka miziki na/au nyimbo na picha (video) zilizo kinyume na maadili ya Kitanzania.
- (x) Kuzuia mahubiri ya aina yoyote na kuzuia kufanya biashara ndani ya basi.
- (xi) Kutunza mazingira kwa kuweka chombo cha kuhifadhi uchafu ndani ya basi.
- (xii) Kusimama sehemu zenye huduma za kijamii kwa angalau dakika 20.

(b) Mabasi ya Mijini (Daladala)

- (i) Nauli zinazotozwa zisizidi ambazo zimetolewa kwenye Tangazo hili.
- (ii) Madereva na wahudumu (makondakta) kuvala sare safi na nadhifu.
- (iii) Mto huduma kutotoza nauli zaidi ya umbali anaoenda abiria.
- (iv) Basi liwe safi wakati wote na kupuliza dawa ya kuua wadudu.
- (v) Nauli ziandikwe ubavuni mwa gari upande wa mlango wa kuingia abiria.
- (vi) Kutokatisha njia (route) ya safari.
- (vii) Kutokuweka miziki na/au nyimbo na picha (video) zilizo kinyume na maadili ya Kitanzania.
- (viii) Kuzuia mahubiri ya aina yoyote na kuzuia kufanya biashara ndani ya basi.

Hivyo, Mamlaka inatoa Notisi ya siku 14 kuanzia tarehe ya kutangazwa kwa taarifa hii, kwamba ye yeyote ambaye hataridhishwa na Amri hii anaweza kukata rufaa Baraza la Ushindani. Baada ya kumalizika siku 14, endapo hakutakuwa na rufaa yoyote, nauli hizi zitaanza kutumika rasmi.

Imetolewa leo tarehe **20 Mwezi Novemba Mwaka 2023.**



AHMED MOHAMED AME
MWENYEKITI WA BODI
MAMLAKA YA UDHIBITI USAFIRI ARDHINI
MAKAO MAKUU - DODOMA